SAVINGS AND CREDIT COOPERATIVE UNION
LEAGUE OF TANZANIA (1992) LTD
SCCULT (1992) LIMITED
S.L.P 20640, Ushirika Buildings Lumumba Road,
16 Floor – Dar es Salaam - Tanzania
Simu: +255 222 185 548/49 | Baruapepe: info@sccult.com

MUHTASARI WA SHUGHULI ZA UTETEZI ZILIZOFANYWA NA SCCULT (1992) LTD KWENYE MASWALA MBALIMBALI KATIKA KUSAIDIA VYAMA VYA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO (SACCOS) NCHINI KWA MWAKA 2020

Na.	SHUGHULI YA UTETEZI	UFAFANUZI	JITIHADA ZA SCCULT (1992) LTD	MIPANGO ENDELEVU
1.	Kodi ya Mapato	Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kupitia Sheria ya Kodi ya mwaka, 2004 walivitaka vyama vya Ushirika kulipa kodi ya mapato kwa asilimia 30 ya faida itakayopatikana kwa mwaka. Mpango huu ulikuwa ni kwa vyama vyenye mapato ghafi (annual turnover) yenye jumla ya shillingi Milioni hamsini 50,000,000 kwa mwaka. Jambo hili lilikuwa changamoto kwa vyama vichanga na kupelekea vyama vingi kushindwa kujiendesha	SCCULT (1992) Ltd iliwasilisha utetezi wake Serikalini kupitia Wizara ya Fedha na Mipango na walikubali kufanya mapitio na kuja na mapendekezo kutoa unafuu kwa kuongeza mapato gafi (annual turnover) kutoka Milioni hamsini 50,000,000/= hadi ya Milioni mia moja 100,000,000/=. Hili lilifanyika kupitia kikao cha Bunge la Bajeti la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi juni mwaka 2020.	SCCULT (1992) Ltd itaendelea kufanya tathimini ya utekelezaji wa Sheria hii na kuangalia kama kuna changamoto zozote kwa kupata maoni na kuwasilisha kwenye mamlaka, pia itahamasisha vyama kulipa Kodi ya mapato kwa wakati ili kuepuka adhabu zisizo za lazima, na kwa faida ya nchi yetu.
2.	Maandalizi ya Sheria namba 10 ya huduma Ndogo za Fedha 2018	Sera ya huduma ndogo za Fedha mwaka 2017 ilielekeza kutungwa kwa Sheria ya usimamizi na udhibiti wa sekta ya huduma ndogo za fedha ikiwemo SACCOS ili kulinda watumiaji wa huduma hizo na kuondoa changamoto zilizokuwepo katika kusimamia sekta hiyo.	SCCULT (1992) Ltd ilishirikiana kikamilifu na wadau mbali mbali kama Wizara ya fedha na Mipango, FSDT, TAMFI, TCDC, BOT kuwa sehemu ya uhamasishaji, kwa vyama ili walishiriki kutoa maoni yao, pia iliishiriki kutoa elimu kwa vyama juu ya mabadiliko hayo ambayo yalipelekea upatikanaji wa Sheria ya Huduma ndogo za fedha 2018, na Kanuni za SACCOS Daraja la III, 2019.	SCCULT (1992) Ltd inaendelea kufanya tathimini ya utekelezaji wa Sheria hiyo na kuelimsha SACCOS kuendana na mabadiliko hayo.
3.	Maandalizi mfumo wa maombi ya leseni	Tume ya Maendeleo ya Ushirika iliandaa mfumo wa maombi ya leseni kwa njia ya mtandao Mfumo wa kuomba leseni kwa njia ya Mtandao uliandaliwa kwa lengo la kusaidia SACCOS kukamilisha mchakato wa maombi ya leseni kwa haraka na urahisi.	SCCULT (1992) Ltd ilishiriki kikamilifu katika mchakato huu kwa kuwezesha kifedha na kutoa maoni ya maboresho ya Mfumo huo **(Kazi hii ilikuwa sehemu ya shughuli zilizofanyika kwenye maandalizi ya Sera za mfano kwaajili ya SACCOS).**	SCCULT (1992) Ltd inaendelea kufanya kazi kwa ukaribu na TCDC na kuendelea kushauri maboresho pale inapobidi.

Na.	SHUGHULI YA UTETEZI	UFAFANUZI	JITIHADA ZA SCCULT (1992) LTD	MIPANGO ENDELEVU
4.	Masharti na Sera za uendeshaji na usimamizi wa SACCOS kwa mujibu wa Sheria ya huduma Ndogo za Fedha	Sheria ya Huduma Ndogo za fedha mwaka 2018, Kanuni za SACCOS, 2019 Daraja la 3 ilikuja na mabadiliko kadhaa katika uendeshaji wa SACCOS, hivyo SACCOS zilitakiwa kuhuisha Sera na Masharti yao ili kuendana na Sheria hii.	SCCULT (1992) Ltd iliratibu mchakato mzima wa maandalizi wa nyaraka za mfano wa Sera na Masharti zinazoendana na Sheria namba 10 ya huduma Ndogo za Fedha, 2018 na Kanuni za SACCOS 2019 na kasha kuzigawa kwa SACCOS. Shughuli ilifanyika kwa kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, COASCO, SACCOS kadhaa, NOSACU.	SCCULT (1992) Ltd itaendelea kusaidia vyama kuhakikisha wanahuisha Masharti yao, na Sera za uendeshaji ili kuendana na Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha
5.	TEHAMA	Sheria namba 10 ya huduma Ndogo za fedha inazitaka SACCOS kuwa na mifumo ya TEHAMA ili kurahisisisha uendeshaji na uchakataji wa taarifa za SACCOS. Hili limeainishwa kwenye Kanuni za SACCOS, 2019 Daraja la III kama kigezo mojawapo katika upatikanaji wa leseni ya huduma Ndogo za Fedha kwa Daraja A na B.	SCCULT (1992) Ltd kwa ushirikiano mkubwa toka kwa wadau imefanya yafuatayo; 1. Imefanya upembuzi yakinifu kwa kushirikiana na wadau kama SBFIC na kuwapendekeza KAMA Digital Solution na Singo Afirika kutoa huduma ya mifumo kwa SACCOS wanachama na zile zisizokuwa wanachama. 2. Kuajiri mtaaalamu atakaye shughulikia masuala yote yahusuyo TEHAMA ndani ya Taasisi na nje ya Taasisi	SCCULT (1992) Ltd itasimamia kwa ukaribu utekelezaji wa takwa hili la kisheria ili kuhakikisha SACCOS zote zinapata mfumo rafiki na kwa gharama nafuu ili kuongeza kasi na tija katika matumizi ya TEHAMA
6.	Huduma za Ukaguzi	Ili kukidhi vigezo vya kupata Leseni ya Huduma Ndogo za Fedha SACCOS zimetakiwa kuajili wakaguzi wa ndani au kuingia mkataba na wakaguzi wa ndani wenye sifa kutegemeana na ukubwa wa chama	SCCULT (1992) Ltd inatekeleza mpango wa kusaidia vyama kuhakikisha huduma hii ya ukaguzi wa ndani inapatikana kwa kuingia ubia na wataalamu wenye weledi na waliothibitishwa na Bodi ya wahasibu (NBAA) watakaotoa huduma hii kwa gharama nafuu na rafiki kwa vyama SACCOS	SCCULT (1992) Ltd itahakikisha huduma hii inatolewa kwa ubora na gharama nafuu ili vyama vyote wapate huduma bila kuangalia uwezo wa chama.

Na.	SHUGHULI YA UTETEZI	UFAFANUZI	JITIHADA ZA SCCULT (1992) LTD	MIPANGO ENDELEVU
7.	Maadhimisho ya Kimataifa ya siku ya Ushirika wa akiba na Mikopo (ICUD)	Kila alhamisi ya tatu mwezi oktoba kila mwaka, huwa ni maadhimisho ya siku ya ushirika wa akiba na mikopo (ICUD), siku hiyo huwakutanisha pamoja wanaushirika na wadau mbalimbali kujadili maswala mbalimbali yanahusu ushirika wa akiba na mikopo. Siku hii huambatana na utoaji wa elimu kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu uendeshaji wa shughuli za SACCOS, tuzo kwa vyama vilivyofanya vizuri baada ya tathimini kufanyika.	SCCULT (1992) Ltd imefanikiwa kuratibu maadhimisho haya na kutumia siku hii kama jukwaa (platform) la kuwakutanisha pamoja wanaushirika na wadau mbalimbali ili kujadili maswala mbalimbali yahusuyo SACCOS na imekuwa kama jukwaa la kukutanisha mamlaka pamoja na wadau na kuja maelekezo/maazimio mbali mbali. Pia siku hii imetumika kama sehemu ya kushindanisha SACCOS na imeleta matokeo chanya. Kwa mwaka 2020 shughuli hizi zimefanyika Jijini Arusha kuanzia tarehe 13 hadi 15 Oktoba	SCCULT(1992) Ltd itaendelea kuratibu siku hii muhimu na kuiboresha zaidi ili iwe na maslahi kwa SACCOS